**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAARIFA YA WILAYA YA RUNGWE KATIKA KUMBUKIZI KUHUSU MAFANIKIO YA MIAKA 61 YA UHURU WA TANZANIA BARA

**TAREHE 09 DISEMBA, 2022**

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru kwa namna ya pekee kwa kufika kwenu kwa wingi. Ni matarajio yangu kuwa kupitia Kongamano hili nina amini mnawakilisha wananchi wengi katika kusherehekea Uhuru wa Nchi yetu pamoja na mafaniko yake . hili litatuwezesha kufahamu kuhusu Mafanikio ya Serikali kupitia Halmashauri ya Wialya ya Rungwe na Busokelo katika Wilaya ya Rungwe wakati huu Taifa likiliadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Pili, nawapongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uzalendo ambao umeiwezesha nchi yetu kuendelea kuwa Taifa lenye amani, umoja na mshikamano, na sasa tunaelekea kuadhimisha miaka 60 ya uhuru tukiwa imara na wamoja kama Taifa

Ndugu wanananchi, kama mnavyofahamu, kila ifikapo tarehe 9 Desemba Nchi yetu huadhimisha uhuru wa Tanzania Bara, na kipekee kwa mwaka huu Serikali imetoa kipaumbele katika kuuhabarisha Umma wa Watanzania na Dunia kwa ujumla kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Miongo sita iliyopita. Kwa muktadha huo nitaeleza kwenu, kwa uchache, mafanikio ambayo Wilaya ya Rungwe imeyapata kupitia majukumu yake ya msingi katika kutoa huduma kwa Wananchi.

## HISTORIA YA WILAYA KWA UFUPI

Ndugu Wananchi, kama ilivyo kwa Wilaya zingine Nchini, Historia ya Wilaya ya Rungwe inaanzia pale Tanzania Bara (wakati huo Tanganyika) ilipopata Uhuru kutoka kwa Uingereza tarehe 09 Desemba 1961. Wilaya ya Rungwe ni moja ya Wilaya 5 na Halmashauri 7 zinazounda Mkoa wa Mbeya. Aidha ni moja ya Wilaya za zamani hapa

nchini kuanzia wakati wa Utawala wa Wajerumani. Wilaya hii iko katika “longitudo 80 30’E na 90 30’E na latitudo 330 S na 340 S.” Wamissionari wengi wa Madhehebu mbalimbali waliingia katika Wilaya hii mwishoni mwa karne ya 19 wakitokea Malawi ambao pamoja na kueneza Dini wametoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya Wananchi hususani katika nyanja za Elimu na Afya. Makao Makuu ya Wilaya yapo katika Mji wa Tukuyu ambao upo kilomita 72 kutoka Makao makuu ya Mkoa wa Mbeya. Katika mji wa Tukuyu huduma zote muhimu kama za Maji, Elimu, Kituo cha Polisi, Mahakama, Gereza, Masoko, Maduka, Hoteli, Kituo cha Mabasi na Mabenki zinapatikana kwa urahisi.

## MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA ELIMU

Elimu ya Msingi

Katika kipindi hiki cha kusherehekea Uhuru wa Tanzania Bara, Wilaya ya Rungwe inajivunia kufanikiwa utekekelezaji wa Lengo kuu la Sekta ya Elimu ambalo ni kusimamia shughuli za Elimu katika mfumo Rasmi na isiyo katika mfumo Rasmi kwa Shule za msingi na vituo vya ufundi stadi. Lengo ni kuboresha Elimu na Mafunzo kwa kuimarisha programu ya mafunzo kazini, kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na kukarabati miundombinu ya shule. Aidha,

Wakati tunapata uhuru mwaka 1961,Wilaya ya Rungwe ilikuwa na jumla ya shule za Msingi 25, miaka 61 baada ya Uhuru wananchi wa Wilaya ya Rungwe wanashuhudia uwepo wa shule za Msingi 213 sawa na ongezeko la asilimia 852.

Sera ya Elimu inasisitiza kushirikisha jamii katika kuendesha na kuziongoza shule. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana baada ya Uhuru ni pampja na:-

### Elimu Sekondari

Wakati tunapata Uhuru Disemba 9,1961, Wilaya ya Rungwe ilikuwa na jumla ya shule MOJA za Sekondari, miaka 61 baadae Wilaya ya Rungwe ina jumla ya Shule za Sekondari 67. Aidha, wakati tunapata Uhuru,Wilaya ya Rungwe ilikuwa na nyumba za

watumishi 17 ambapo kwa sasa kuna jumla ya nyumba za walimu 92. Mabweni yameongezeka kutoka 5 hadi kufikia mabweni 29.

Aidha, wakati tunaadhimisha miaka 61 ya Uhuru, na kuhakikisha elimu ya Sayansi na Teknolojia inakuzwa kwa wananchi ili kuongeza tija katika matumizi ya rasilimal zetu, jumla ya maabara 96 zimejengwa ikilinganishwa wakati tumepata Uhuru Wilaya ilikuwa haina maabara hata moja katika shule ya Sekondari moja iliyokuwepo katika kipindi hicho.

Matokeo ya uboreshaji wa sekta ya Elimu ya Sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imeweza kufanikiwa katika maeneo yafuatayo:-

i. Idadi ya walimu wa sekondari imeongezeka kutoka walimu 527 katika kipindi cha miaka ya 10 iliyopita hadi walimu 944 waliopo kwa sasa. Hili ni ongezeko la asilimia 45
ii. Idadi ya wanafunzi wanaofaulu na kujiunga kidato cha tano imeongezeka kutoka asilimia 42 miaka 10 iliyopita hadi asilimia 65.7 mwaka 2021.
iii. Idadi ya wanafunzi wanaofaulu na kujiunga kidato cha kwanza imeongezeka kutoka asilimia 80 hadi asilimia 92 sawa na ongezeko la asilimia 12

**KATIKA SEKTA YA AFYA**

Katika kipindi hiki ambacho tuaadhimishi siku ya Uhuru wa Tanzania Bara, napenda kuwakumbusha wananchi wakati tuna pata Uhuru mwaka Disemba 9,1961, Wilaya ya Rungwe ilikuwa haina hospitali na vituo vya Afya isipokuwa ilikuwa na Zahanati 4 tu. Leo wakati tunaadhimisha miaka 61 ya Uhuru, Wilaya ya Rungwe ina Hospitali 4, zahanati 64 na vituo vya afya 9.

**MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI**

**Utangulizi**

Huduma ya maji kabla ya uhuru ilikuwa inapatikana katika mji wa Tukuyu mjini tu ambapo kulikuwa na mradi unaotumia teknolojia ya Pampu ya Dizeli tokea chanzo cha maji kiitwacho Lubalisi kilichopo Mabonde chini ya eneo la Chibwaya. Huduma ya maji Wakati huo ililenga kuwafikia Watumishi na maofisa wa Serikali na Wananchi wa jirani ambapo walipata maji kupitia vioski vilivyokuwa katika mgawanyo ufuatao; Bulyaga kioski kimoja, Bagamoyo vioski vitatu (ikiwemo soko mjinga mwisho wa mji), Kiwira Road kioski kimoja (mwisho wa kota ya posta) na Sokoni kioski kimoja

**Maji Vijijini**

Halmashauri inafanya jitihada za kuwapatia wananchi waishio vijijini maji safi na salama karibu na makazi yao ndani ya umbali wa mita 400 kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya maji ya mwaka 2002. Asilimia 74.4 ya wananchi waishio Vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama.

Baada ya Uhuru, Serikali imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanapata maji katika maeneo yao ambapo miradi ya maji ya Lwangwa (1968), Ushirika (1968), Masukulu, Kiwira na Ngopyolo. Katika kutekeleza azma hiyo, miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa na Serikali katika Wilaya yetu ni miradi ya maji ya Lukata, Malangali, Mpandapanda, Ikuti-Lyenje, Kanyelele, Kandete, Isaka n.k hata hivyo miradi inayoenda kuanza kutekelezwa katika Wilaya yetu ni Ukarabati wa mradi wa maji Kabembe group, Ujenzi wa mradi wa maji Kikota, Ntaba, Masoko II na mradi wa maji Idweli

**Maji Mjini**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tukuyu ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa tarehe 21/08/2002 na ilitangazwa kwenye gazeti Namba 258 kuwa Mamlaka ya daraja C. Lengo la kuanzishwa kwa Mamlaka ni kwa ajili ya kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa mji wa Tukuyu. Baada ya Mamlaka kuanzishwa ilianza kuhudumia wakazi wa mji wa Tukuyu kwa kupitia mifumo ya maji iliyopo ambayo

ilijengwa kipindi cha miaka ya 1957 na 1960 ambayo ndiyo mifumo ya maji inayotumika hadi sasa katika Kata 6 ambazo ni Makandana, Kawetele, Ibighi, Bulyaga, Bagamoyo na Msasani ambapo kwa sasa asilimia 80 ya wakati wa Tukuyu mjini wanapata huduma ya maji na kwa sasa kuna mradi wa maji unaendelea kujengwa ili kuboresha upatikanaji wa maji mjini ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.

## SEKTA YA BARABARA TARURA RUNGWE

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 765.91.Kati ya hizo kilomita 16.85 ni barabara za LAMI, kilomita 283.23 ni barabara za Changalawe na kilomita 465.83 ni barabara za Udongo,kilomita 55.0 ni barabara zilizo tengenezwa na kukarabatiwa Pamoja na ujenzi wa madaraja mawili umekamilika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikiwa ni matengenezo ya mara kwa mara kwa jumla ya Tshs. 921,075,149.47. Aidha kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Tshs.1,911,225,455.68 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kilomita 106.29 na madaraja mawili ambapo mpaka Juni 2022 jumla kilomita 106.29 zimetekelezwa(kwa kiwango cha Changalawe kilomita 13.5 na kuchonga barabara kilomita 92.79). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Tshs 1,911,225,455.68 kimetengwa kwa ajili ya kutengeneza kilomita 49.02 barabara za Changalawe na madaraja matatu.

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya miradi tangu kuanzishwa kwa TARURA:-

i. Ujenzi wa Daraja la mdomo mmoja katika Barabara ya Bulyaga - Kyara – Nditu katika mwaka wa fedha 2017/2018.
ii. Ujenzi wa barabara ya Bomani – Msasani yenye urefu wa (1.2km) Kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2017/2018.
iii. Ujenzi wa barabara ya Kiwira Rd - Ndembela yenye urefu wa (0.8km) kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2018/2019.
iv. Ujenzi wa barabara ya Keepleft - Sabato (0.3km), Sabato - Tandale (0.3km) na barabara ya Kyela Road - Pccb (0.1km) kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2018/2019.

v. Ujenzi wa barabara ya Masebe DSP-Mpuguso TTC-Bugoba Kibaoni (5km) kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2018/2019.
vi. Ujenzi wa barabara ya Masebe – Bugoba - Lutete (7.44km) kwa kiwango cha lami kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
vii. Ujenzi wa daraja la Isaka katika kata ya Nkunga na daraja la Mgojo katika kata ya Lupepo katika mwaka wa fedha 2020/2021.
viii. Upandishwaji hadhi kwa kiwango cha changarawe katika barabara ya Masukulu – Kikole (7.5km) na ujenzi wa daraja la midomo miwili katika mwaka wa fedha 2021/2022.
ix. Matengenezo ya muda maalumu katika barabara ya Ntokela – Swaya na ujenzi wa daraja la mdomo mmoja katika mwaka wa fedha 2022/2023.
x. Matengenezo ya muda maalumu katika barabara ya Ibungu – Kyobo Juukwa kiwango cha changarawe katika mwaka wa fedha 2022/2023.
xi. Matengenezo ya muda maalumu katika barabara ya Stamico - Ngubati Ps - Lutetena barabara ya Mwambegele - Tukuyu Spring Water- Lupoto kwa kiwango cha changarawe katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA KILIMO**

1. Utangulizi:

Kilimo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya wilaya ya Rungwe ambapo zaidi ya asilimia 90 ya pato lote la Wilaya linatokana na Kilimo. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 92,389.5. Wilaya inatilia mkazo ongezeko la uzalishaji kwa hekta (tija) kutokana na maeneo madogo yaliyopo kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Kuhifadhi Ardhi, Maji na Mazingira. Sekta ya kilimo imepitia hatua mbalimbali tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Kumekuwa na mabadiliko ya sera ya kilimo ambapo kwasasa sera ya Kilimo ya Mwaka 2003 inaweka mkazo katika mambo yafuatavyo;

- kuanzisha na kuchangia katika Ukuaji wa viwanda hususani viwanda vya kusindika mazao

- Kuzalisha ajira kwa wananchi hususani jeshi kubwa la vijana wanaohitimu masomo katika ngazi zote.
- Kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi na kipato cha wanchi
- Kuchangia katika suala zima la uhakika wa chakula na lishe

## 2.0 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA KILIMO

- Katika mwaka 1961 Wilaya haikuwa kituo hata kimoja cha Kilimo  kwa sasa tuna kituo kimoja cha raslimali cha Kilimo cha Ilenge

- Katika mwaka 1961 kilimo cha viazi kilikuwa cha kujikimu kwa sasa 2022 maendeleo ya kilimo yametokea ambapo kilimo cha viazi ni cha kibiashara ambapo sehemu kubwa (zaidi ya 70%) inayozalishwa ya zao hili ni kwa ajili ya soko la nje ya wilaya.

- Katika mwaka 1961 Kilimo cha Chai kilikuwa ni cha makabaila (mabepari) wa kikoloni kwa sasa(2022) kiasi kikubwa cha zao hili kinachangiwa na wazalishaji wadogowadogo (smallholder famers) ambao wanachangia asilimia 70 ya uzalishaji wote wa zao hili na sehemu inayobaki inazalishwa na makampuni binafsi.

- Katika mwaka 1961 hakikuwepo kilimo cha zao la matunda ya maparachichi ambapo kwa sasa zao hili ni zao muhimu la kibiashara wilayani Rungwe.

- katika mwaka 1961 ruzuku ya mbolea kutoka serikalini kwa ajili ya wakulima haikuwepo kwa sasa serikali inatoa ruzuku kwa ziadi ya tani 13,000 za mbolea.

Vilevile, Wilaya itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi  kuongeza ushiriki wake katika masuala ya uwekezaji kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji kuendelea kutoa mchango wao katika maendeleo ya Wilaya na Taifa kwa ujumla; na kuendelea kuziwezesha mamlaka za serikali za mitaa ngazi za chini kutekeleza kikamilifu majukumu yake hususani usimamizi wa shughuli za maendeleo na kijamii.

Ndugu Wananchi, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana kwa mwitikio wenu, na ni matarajio yangu kuwa mtatumia kongamano hili kueneza taarifa ya mafanikio ya Serikali kupitia shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Serikali kupitia Halmashauri zake katika kipindi cha miaka 61 ya uhuru kwa Wananchi.

Ndugu Wananchi, nimalizie kwa kuwasilimu tena kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……Kazi iendelee!!!

Asanteni kwa kunisikiliza.